**MKATABA WA KUPANGISHA GODOWN**
**(LEASE AGREEMENT)**
**ILIYOPO: KIWANJA Na 48 'KITALU '.......' KAGONGWA INDUSRIAL AREA KAHAMA-MANISPAA-SHINYANGA.**

Umefanyika leo tarehe ...11..... Mwezi ..07....Mwaka 2024

kati ya

**PETER METHIEW SWAI** wa P. O. Box 406 KAHAMA SHINYANGA ambaye kwenye Mkataba huu atajulikana kama **MWENYE GODOWN** , jina ambalo litamaanisha kila mahali ambapo maudhui yake yataruhusu (yaani: Watendaji, Watawala na Wawakilishi wa pande zote).

**NA**

**CELEDES COMPANY LIMITED** wa P. O. Box Kahama Shinyanga ambaye atajulikana hapa kwenye Mkataba huu kama **MPANGAJI** – jina ambalo litamaanisha mahali pote ambapo maudhui yake yataruhusu hivyo – (yaani Watendaji, Watawala na Wawakilishi wa pande zote).

**MWENYE GODOWN** na **MPANGAJI** kwa pamoja wanashuhudia:

1. **KWAMBA:**

(a) **GODOWN** limempangishwa kwa kipindi cha miezi kumi na mbili ( MWAKA MMOJA TU) kuanzia tarehe 11/07/2024 hadi tarehe 10/07/2025 kwa gharama ya Milioni ishirini na tano tu ( Tsh 25,000,000/=) na si vinginevyo.

(b) **KODI YA PANGO** katika GODOWN tajwa hapo juu imelipwa yote kwa mkupuo mmoja leo hii tarehe 11/07/2024 ambapo kiasi cha Tsh 25,000,000/= kimelipwa kwa MWENYE GODOWN.

(c) **MPANGAJI** amempatia MWENYE GODOWN kiasi tajwa hapo juu na MWENYE GODOWN anakiri kupokea kiasi cha Tsh25,000,000/= kwa malipo ya miezi kumi na mbili tu (MWAKA MMOJA).

2. **MAKUBALIANO MENGINE NI KWAMBA:**

i) **MPANGAJI** atatumia GODOWN hilo kwa ajili ya kuhifadhi mali zake, hivyo hataweka kwenye Godown hilo vitu vyovyote vya aina ya milipuko ambapo kuwepo kwake kunaweza kuhatarisha usalama wa watu na mali kwa namna moja au nyingine

ii) **MPANGAJI** ataheshimu sheria zote na taratibu halali zinazokubalika na jamii ili kudumisha usalama wa watu na mali zao.

iii) **MPANGAJI** ataweka GODOWN hilo katika hali ya usafi wa kuridhisha nje na ndani; ikiwa ni pamoja na utunzaji wa kuta, milango, madirisha, nyaya na vifaa vya Umeme ambavyo ni **MALI YA TANESCO** vilivyomo kwenye GODOWN.

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

makubaliano mapya na **MWENYE GODOWN** kwa namna ambayo wataafikiana wakati huo.

uthibitisho: Kwa kuthibitisha hayo hapo juu pande zote mbili zimeridhika zimekubaliana kuweka saini zao wakiwa na akili timamu bila kushurutishwa/kushawishiwa/kulazimishwa na Mtu yeyote yule Mbele ya Kamishna wa viapo na Mashahidi wao Leo hii tarehe……… Mwezi…………2024.

Mkataba huu umesainiwa na kutolewa na
**PETER METHIEW SWAI**
ambaye namfahamu/ ametambulishwa kwangu
……………………………………….ambaye namfahamu
Leo tarehe……Mwezi…………2024

………………………………
**MWENYE GODOWN**

**SHAHIDI**
JINA: GODFREY T. MARUHE
ANUANI 2046 KAHAMA

…………………
**SAINI**

Mkataba huu umesainiwa na kutolewa na
**CELEDES COMPANY LIMITED**
ambaye namfahamu/ ametambulishwa kwangu
……………………………………….ambaye namfahamu
Leo ……………..Mwezi wa ……2024

CELEDES COMPANY LIMITED
MBANGAJI
Mob: +255 757 910 242
KAHAMA-SHINYANGA

**SHAHIDI**
JINA: NIYONKURU DESIRE
ANUANI: 0757 910 242
PASSPORT NO: PC 647 657
CHEO; MKURUGENZI

…………………
**SAINI**

**SHAHIDI**
JINA: NDORIMANA CELESTIN
ANUANI: 0760 825 391
PASSPORT NO: PC 635 708
CHEO; MKURUGENZI

…………………
**SAINI**

**MBELE YANGU**

JINA FESTO DANIEL LEMA

SAINI ……………………

TAREHE…… 11/07/2024

CHEO…… WAKILI

**KAMISHINA WA VIAPO**

iv) **MPANGAJI** haruhusiwi kumpangisha au kubadilishana upangaji na mtu mwingine (kupasiana pango au Ku-sub-let) **GODOWN** /Nyumba/**GODOWN** aliyopangishwa, pia asije akafanya matengenezo yoyote ya kiujenzi katika **GODOWN** hilo bila ya kushauriana na kupata kibali kutoka kwa **MWENYE GODOWN** .

v) **MPANGAJI** atamruhusu **MWENYE GODOWN, MAMLAKA YA MAJI** au/na **MAOFISA WAKAGUZI WA LUKU** kutoka **TANESCO** kuingia muda na wakati unaofaa (official hours) kuona na kufanya matengenezo yatakayohitajika baada ya kutoa taarifa kwa **MPANGAJI** au **MWAKILISHI WAKE** ili mradi matengenezo hayo hayatachukua muda mrefu au kusababisha uhamishaji wa vifaa Ndani ya **GODOWN** .

vi) **KWAMBA** Mpangaji atawajibika kutunza **GODOWN** hicho wakati wote wa mkataba huu na atawajibika katika ukomo wa mkataba huu kukabidhi **GODOWN** alivyopangishwa likiwa katika hali nzuri inayoshabiana na wakati huu anapopangishwa.

vii) **KWAMBA** Mwenye **GODOWN** ameridhia Mpangaji afanye matengenezo madogo madogo kwenye **GODOWN** hicho kwa wakati wote wa mkataba huu na matengenezo haya kama yapo hayatabadilisha ama kusudia kubadilisha chochote kwenye muonekano wake wa sasa.

viii) **MPANGAJI** atalipa Maji/umeme (**LUKU**) kulingana na matumizi yake kwa muda unaohitajika.

3. **VILE VILE IMEKUBALIWA NA KUTAMKWA KWAMBA:**

(i) Endapo **MPANGAJI** atanuia kuendelea kupanga **GODOWN** hicho kwa kipindi kingine baada ya kipindi cha Mkataba huu kumalizika, na ikiwa nia yake ipo, atampa **MWENYE GODOWN** taarifa ya angalau siku thelathini [30 days] kabla ya kumalizika kwa kipindi kilichokubaliwa katika **MKATABA** huu na wataweka mkataba mpya ambao utakuwa na makubaliano mapya na si vinginevyo.

(iii) *Mpangaji* atahakikisha kuwa haachi malimbikizo yoyote ya Ankara zozote endapo atahitaji kutoendelea na Mkataba. Na iwapo Mpangaji atakatisha mkataba huu kabla ya muda wake kwisha hatakuwa na haki ya kudai chochote ikiwa ni pamoja na kodi ya pango ambayo haijatumika **VILEVILE** Mwenye **GODOWN** akitaka kukatisha mkataba kabla ya muda atatoa notisi ya kusudio ambalo siyo chini ya miezi mitatu na atawajibika kurudisha kodi yote ambayo haijatumika kulinga na ukomo wa mkataba

(iv) **MKATABA** huu utaishia tarehe 09/07/2025 Endapo **MPANGAJI** atapenda kuendelea kupanga **GODOWN** hilo, na atakuwa ameonyesha nia hiyo kama ilivyo kwenye Kifungu Namba 4(1) juu, itabidi kufanya

Scanned with
CamScanner

Scanned with
CamScanner